TANGAZO LA SERIKALI NA. 750 la tarehe 23/8/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikama kama Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"choo" maana yake ni chumba maalumu ambacho kimejengwa ambacho kitakuwa na shimo pembeni kwa ajili ya kuhifadhia kinyesi au mkojo wa binadamu;

"chombo cha taka" maana yake ni chombo cha kuwekea taka kinachoweza kuhamishika, chenye mfuniko unaofunga vizuri na mishikio;

"eneo la hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa

ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"kamati"-

(a) inapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Kijiji ina maana ya Kamati iliyoanzishwa au iliyoteuliwa na Halmashauri ya Kijiji.

(b) inapotumika kuhusiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata ina maana ya Kamati hiyo; na

(c) inapotumika kuhusiana na Kamati nyingine ina maana ya Kamati hiyo;

"kiwanda" maana yake ni jengo au majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa misitu, visiki;

"maeneo ya malisho" maana yake ni maeneo yaliyotemgwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri kwa ajili ya malisho;

Sura ya 191

"maji" yatakuwa na maana kama kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191

"maji taka" yatakuwa na maana kama yalivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 323

"mazao ya misitu" yatakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

Sura ya 191

"mazingira" yatakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anaejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni mnyama yeyote inayofugwa na binadamu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"Mwenyekiti"-

(a) inapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya.

(b) inapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Kijiji

maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji.

(c) inapotumika kuhusiana na kamati, maana yake ni Mwenyekiti wa kamati;

Sura ya 191

"taka" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka ngumu" zitakuwa na maana kama zilivyotafsiwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"taka za viwandani" zitakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

"uchafu hatari" utakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa Halmashauri

4.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malisho ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kufuga idadi ya mifugo itakayoamriwa na Halmashauri husika;

(b) kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(c) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(d) kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;

(e) kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

(g) kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(h) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(i) kuweka alama kwenye mifugo yake na katika

viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
(j) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri;
(k) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o; na
(l) kusajili mifugo katika rejista ya kijiji, kuogesha mifugo katika majosho kama ratiba itakavyopangwa.

Marufuku kwa mfugaji

6. Itakuwa marufuku kwa mfugaji yeyote:
(a) kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;
(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani zaidi ya kilometa thelathini;
(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali kitakachotolewa na Halmashauri;
(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri; na
(f) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

7.-(1) Halmashauri itakamata mfugo wowote utakaoonekana unazurura katika eneo la Halmashauri ambalo halijaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa mahali pasipostahili utalipiwa faini ya Shilingi elfu ishirini kwa kila mfugo baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo.

(5) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo

Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa na uzembe wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo

8.-(1) Maafisa mifugo wa Halmashauri au Afisa Mwidhiniwa atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii ataweza kuingia katika maboma au jengo lolote wakati wa muda wa kazi kwa madhumuni ya kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayewazuia Maafisa Mifugo au Afisa Mwidhiniwa katika kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii anatenda kosa.

Taratibu za ufugaji

9.-(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote inayohusu utaratibu wa ufuigaji.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kuchinja mifugo yake machinjioni au mahali palipotengwa kwa ajili ya huduma hiyo.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

(4) Itakuwa marufuku kwa mbwa na nguruwe kuachiliwa wakizurura, Mbwa watatakiwa kufungiwa kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi na kuachiwa Saa nne kamili usiku.

Taratibu za kilimo

10.-(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo zilizoainishwa kwenye sheria na kanuni mbalimbali.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo kuingia katika shamba lolote wakati wa muda wa kazi kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Makatazo

11. Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira.

(b) kutumia ardhi kinyume na matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(c) kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.

(d) kutupa mabaki ya vifungashio vya Viuatilifu, kusafisha vipulizi au kumwaga mabaki ya viuatilifu katika vyanzo vya maji yanayotiririka au mito.

(e) kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa Halmashauri.

(f) kutumia mifuko ya plastiki katika eneo lote la Halmashauri na matumizi ya vifungashio vya mifuko ya plastiki kama vibebeo.

(g) kutumia mifuko mbadala isiyokidhi viwango na kuwa na alama ya inayooneshwa kuthibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania.

(h) kujenga nyumba kiholela au kujenga jengo lolote katika eneo la hifadhi bila kibali cha Halmashauri.

Uchimbaji mchanga na kokoto

12. Mtu hataruhusiwa-

(a) kuchimba mchanga, kifusi au kuchoma tofali katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa, kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri;

(b) kujenga nyumba, jengo lolote au kufanya shughuli zozote za kiuchumi katika eneo la hifadhi; na

(c) kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji bila kuwa na kibali maalum kutoka Halmashauri.

Uhifadhi wa uoto wa asili

13. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti ili kutoendelea kuharibu mazingira na kurejesha uoto katika hali yake ya asili.

Wajibu wa Halmashauri kulinda vyanzo vya maji

14.-(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila

sababu ya msingi.

(3) Halmashauri na jamii husika itakuwa ni wajibu wa kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

Kulinda eneo la hifadhi

15. Mtu yeyote hataruhusiwa kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

16. Mtu, kiwanda, taasisi au shirika lolote haliruhusiwi-

(a) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai; au

(b) kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

Kuchoma au kusababisha moto

17.-(1) Mtu hataruhusiwa kuchoma au kusababisha moto katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Kila mwananchi atakuwa na wajibu wa kuzima moto ambao utaonekana kuwaka katika eneo la Halmashauri yenye kuleta viashiria vya hatari.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Ukataji miti

18.-(1) Mtu hataruhusiwa-

(a) kukata miti katika maeneo ya misitu iliyofadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri; na

(b) kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe hai maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(2) Afisa Misitu atahakikisha miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa

watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

19. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika-
(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;
(b) kupanda na kutunza miti katika makazi yake; na
(c) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki;

Utupaji wa taka ngumu na laini

20.-(1) Halmashauri itatenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo husika.

(2) Mtu atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo za mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa anatenda kosa.

(3) Taka zote katika eneo la Halmashauri zitatupwa katika eneo maalum au jalala kuu lililotengwa au litakalotengwa na Halmashauri kwa ajili hiyo na Halmashauri itawajibika kusimamia usafi katika eneo lake.

(4) Kila Kaya, eneo la biashara, ofisi, Karakana na vyombo vya usafiri wa abiria lazima viwe na chombo cha kuhifadhia taka ndani ya eneo la mji na katika maeneo ya vijijini lazima yawe na mashimo ya taka nyuma ya nyumba.

(5) Kila mtu anawajibu wa kuwa na choo salama, na kwa misingi hiyo si ruhusa kwa mtu kujisaidia haja ndogo au kubwa, au kumwaga mkojo, kinyesi au matapishi katika mtaa, eneo la jamii, uchochoroni, njiani, barabarani, sehemu yoyote au katika eneo lolote isipokuwa katika choo na kwa kuzingatia usafi wa choo hicho.

Uendeshaji wa viwanda, vituo vya mafuta, huduma za ujenzi

21.-(1) Mtu anayeendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu atatakiwa kuzingatia taratibu za ujenzi.

(2) Endapo mtu atataka kuendesha shughuli za viwanda, vituo vya mafuta, vituo vya huduma mbalimbali za ujenzi atatakiwa kuzingatia tahadhari ya athari za mazingira.

(3) Mtu yeyote akienda kinyume na kanuni ndogo ya (1) na (2) atakuwa anatenda kosa.

Jukumu la kaya kuvuna maji ya mvua

22.-(1) Kila kaya itakuwa na jukumu la kuweka utaratibu wa kuvuna maji ya mvua wakati wa kipindi cha mvua ili kukabiliana na ukame wakati wa kipindi cha kiangazi.

(2) Kaya hizo zitaandaa mpango wa uvunaji maji hayo katika hali ya usafi kwa kuzingatia afya ya mtumiaji na jamii kwa ujumla.

(3) Kila Taasisi, Shule za Msingi, Sekondari, Zahanati na Vituo vya Afya vitakuwa na wajibu wa kuweka miundo mbinu ya kuvuna maji ya mvua kwenye mapaa ya majengo yao kwa faida ya kutumia maji kwa jamii.

(4) Mmiliki wa ardhi yoyote atakuwa na haki ya kujenga miundo mbinu ya uvunaji wa maji ya mvua na kuhifadhi maji hayo kwa matumizi ya nyumbani.

(5) Hakutakuwa na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ambayo itakuwa na uwezo zaidi ya uwezo wa kanuni zilizotolewa na mamlaka husika.

Uhifadhi wa korongo

23. Kila mwananchi atakuwa na jukumu la kuhifadhi makorongo yote yanayopitisha maji katika msimu wa mvua, na kuyalinda kwa kuacha mita 60 kutoka kila upande wa kingo ya korongo ili mradi liwe linapeleka maji kwenye bwawa kwa matumizi ya binadamu, kilimo na mifugo.

Wajibu wa kuweka miundombinu ya kuvuna maji kwenye mchoro

24.-(1) Kila mwenye ardhi anayetaka kujenga nyumba au jengo la biashara au makazi ni lazima katika michoro yake abainishe na kuonyesha miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

(2) Usanifu, uratibu na usimamizi utazingatia miongozo, kanuni na viwango vilivyopendekezwa au vilivyoainishwa na Serikali kupitia miongozo mbalimbali.

(3) Mchoro ambao hautaonyesha na kubainisha miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua utakuwa ni batili na hautopitishwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi hadi hapo utakapoonyesha na kubainisha miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

(4) Wakati wowote Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi na ikiihusisha Idara ya Maji itafanya ukaguzi kuhakikisha kuwa nyumba zote zilizojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, zinajengwa na miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua na miundombinu hiyo inatumika baada ya

ukamilikaji wake.

Makosa

25. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:
(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali;
(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;
(e) atakiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, mawe kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
(f) ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;
(g) atachoma au kushiriki katika kuanzisha moto au, hatashiriki katika shughuli ya kuzima moto bila ya sababu ya msingi;
(h) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa au isiyohifadhiwa bila kibali;
(i) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;
(j) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka, na kung'oa visiki katika misitu bila kibali;
(k) atatupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(l) atajisaidia haja kubwa au ndogo sehemu isiyo kuwa chooni au atatupa uchafu wa aina hiyo mahali pasipostahili au mahali ambapo siyo chooni;
(m) atatiririsha maji machafu yanayoweza kuleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai;
(n) ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, kituo cha kuoshea magari, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
(o) atachafua maji yaliyohifadhiwa kwa matumizi ya baadae na kusababisha madhara kwa watu, mifugo, mazao, bustani na mazingira ambayo yanamwagiliwa na maji hayo au kwa njia yoyote ile ambayo italeta uharibifu na uchafuzi kwa kutumia maji;

(p) mkuu wa taasisi au kaya zitakazoshindwa kuweka utaratibu wa kuvuna maji ya mvua watakuwa wamevunja taratibu zilizoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(q) atamzuia kwa namna yoyote ile mtumishi wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(r) atauza, atanunua, atasambaza au kutumia mifuko ya palastiki; na

(s) ataendesha kaya, ofisi, eneo la biashara, karakana ambayo haina chombo cha kuhifadhia taka katika eneo la mji.

Adhabu

26. Mtu anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote.

Kufifilisha kosa

27. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo T.S Na. 121 la 2012

28. Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira na Vyanzo vya Maji za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza zinafutwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina…………………….……………………….. Saini…………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………………
Saini……………………….……………………….………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe…………………………

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 07 Mwaka 2022 na lakari hiyo ilibandikwa mbele ya;-

DR JUMAA MOHAMED MHINA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya Muheza*

ERASTO JEROME MHINA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Muheza*

NAKUBALI,

/

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*